


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MADINI

TUME YA MADINI



Telegramu "**MADINI**"
Simu: + 255-26 2320051
Nukushi: +255 26 2322282
Barua pepe: ceo@tumemadini.go.tz

S. L. P. 2292,
DODOMA

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Ndugu waandishi wa habari, *'Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania'* Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia kukutana katika siku hii tukiwa hai na wenye afya njema.

Ndugu waandishi wa habari, Tume ya Madini imeendelea kuongeza kasi ya utoaji wa leseni kwa kuimarisha Mfumo wa Utoaji na Usimamizi wa Leseni za madini. Kutokana na kasi hiyo, Tume ya Madini imeendelea kuwa na mwenendo chanya katika utoaji wa leseni za madini ambapo Mwaka 2018/2019 zilitolewa jumla ya **leseni 5,094**; Mwaka 2019/2020 **leseni 7,214** na Mwaka 2020/2021 zilitolewa jumla ya **leseni 7,862**. Takwimu hizi zinathibitisha ukuwaji wa Sekta ya Madini.

Ndugu waandishi wa habari, baadhi ya makampuni na watu binafsi walioaminiwa na Serikali na kupewa leseni wameshindwa kutekeleza masharti ya leseni kwa mujibu wa Sheria ya Madini Sura ya 123 ikiwa ni pamoja na **kulipa ada za leseni na kuziendeleza leseni zao**. Hadi kufikia tarehe 26 Julai, 2021, jumla ya **leseni 443** za utafutaji madini zinadaiwa jumla ya **Shilingi Bilioni 9.31** zilizotokana na malimbikizo ya ada za mwaka za leseni hizo tangu zilipotolewa hadi sasa.

Ndugu waandishi wa habari, mtakumbuka kuwa Waziri wa Madini Mhe. Dotto Biteko (Mb.) katika nyakati tofauti ameendelea kuielekeza Tume ya Madini na kuwahamasisha wawekezaji kuhakikisha

wanaendeleza maeneo yao na kulipia ada stahiki za leseni zao. Lengo la Mhe. Waziri ni kuhakikisha kuwa wawekezaji wanapatiwa taarifa za ziada mapema kabla ya hatua za kisheria kama hizi hazijachukuliwa. Nawasihi wawekezaji wote nchini kuhakikisha wanafuata maelekezo ya Mhe. Waziri na viongozi wengine wa Serikali wakati wote.

Ndugu waandishi wa habari, napenda kuchukua fursa hii, kuwaomba wamiliki wote wa leseni ndani na nje ya nchi kulipia leseni zao **ndani ya siku 60** kinyume na hapo hatua za kisheria zitachukuliwa ikiwa ni pamoja **na kufuta leseni** hizo na wahusika **kufikishwa mahakamani**. Ikumbukwe kuwa, lengo la Serikali sio kufuta leseni za wawekezaji bali ni kuhakikisha kuwa sheria, kanuni na taratibu zote zilizowekwa na nchi zinafuatwa na kutekelezwa.

Ndugu waandishi wa habari, nichukue fursa hii pia kuwaelekeza Maafisa Madini wote nchini kufuta leseni zote ambazo hazijaendelezwa na ambazo hazijalipiwa ada ya mwaka kwa mujibu wa Sheria ya Madini Sura 123 baada ya **siku 60** kuanzia tarehe ya tangazo hili.

Ndugu waandishi wa habari, orodha ya leseni zote ambazo hazijaendelezwa na ambazo hajizalipiwa ada ya mwaka zinapatikana kupitia tovuti ya Tume ya Madini, (www.tumemadini.go.tz).

Asanteni kwa kunisikiliza.

Imetolewa na:



Prof. Idris S. Kikula

MWENYEKITI WA TUME YA MADINI

27.07.2021